THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL
CERTIFICATE OF SECONDARY EDUCATION EXAMINATION

015/2

ELIMU YA DINI YA KIISLAMU 2

(Kwa Watahiniwa Walioko na Wasiokuwa Shuleni)

Muda: Saa 2:30 **Ijumaa, 19 Oktoba 2012 mchana**

Maelekezo

1. Karatasi hii ina sehemu A, B, C na D.
2. Jibu maswali **manne (4),** swali **moja (1)** kutoka kila sehemu.
3. Kila swali lina alama 25.
4. Simu za mkononi **haziruhusiwi** katika chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

Scanned by CamScanner

BISMILLAHIR - RAHMANIR - RAHIIM

SEHEMU A: QUR'AN

1. *Hawazingatii nini, hii Qur-an? Na kama ingelitoka kwa asiyekuwa Mwenyezi Mungu bila shaka wangalikuta ndani yake khitilafu nyingi (4:82).*
   Kwa kurejea Qur'an, toa hoja nane kuthibitisha kuwa Qur-an ni kitabu cha Allah (s.w).

2. Andika tafsiri ya suratul-A'laa (87:1-19) na kisha elezea mafunzo saba ya jumla yatokanayo na sura hii.

3. Wapinzani wa zama hizi nao wametoa madai kadhaa katika kuipinga kwao Qur'an, miongoni mwa madai hayo ni:
   (a) Muhammad alitunga Qur'an ili kuleta umoja na ukombozi wa Waarabu.
   (b) Kurekebisha tabia za Waarabu.
   Jadili sababu sita zinazoonesha udhaifu wa wapinzani hao. Sababu nne kutoka kipengele (a) na sababu mbili kutoka kipengele (b).

SEHEMU B: TAWHIID

4. *Kwa hakika Tuliwapeleka Mitume kwa dalili waziwazi (57:25).* Bainisha dalili sita za kuwepo Mwenyezi Mungu zinazodhihirishwa na historia ya maisha ya mitume.

5. Jadili hoja sita kwa mujibu wa Qur'an kufafanua taathira ya kuamini Malaika katika maisha ya kila siku.

6. Kwa kuzingatia hali halisi ya maisha ya jamii na Qur'an, eleza sababu sita zinazolazimu iwepo siku ya malipo.

SEHEMU C: FIQH

7. *"Na mtoto mwanamke aliyezikwa hali ya kuwa yu hai atakapoulizwa kwa makosa gani aliuliwa?" (81:8-9).* Kwa kuzingatia aya uliyopewa na aya nyingine kutoka kwenye Qur'an na Sunnah, ainisha haki nane za mwanamke zitolewazo na Uislamu.

8. *Kila mmoja wenu ni mchunga na ataulizwa juu ya wale au vile alivyokuwa akivichunga. (Mtume s.a.w).*
   (a) Jadili aina tano za amana katika maisha ya jamii kwa mujibu wa Uislamu.
   (b) Onesha jinsi Mtume (s.a.w) alivyokuwa mchungaji mzuri wa amana.

9. Kwa kuzingatia aya ifuatayo: *"Enyi mlioamini! Mmelazimishwa kufunga (Saumu) kama walivyolazimishwa waliokuwa kabla yenu ili mpate kumcha Mungu" (2:183.).*
   (a) Toa maelezo mafupi juu ya umuhimu wa funga ya Ramadhan katika Uislamu na kwa nini imefaradhishwa mwezi wa Ramadhan.
   (b) Jadili vipengele sita vinavyoonesha jinsi funga inavyomuandaa Muislamu kuwa mcha mungu.

Scanned by CamScanner

SEHEMU D: TAREKH

10. Jadili mbinu nane za makafiri wa Makka walizotumia katika kuzima nuru ya Uislamu wakati wa Mtume (s.a.w).

11. Bainisha mitihani mitano aliyopewa Nabii Ibrahim (a.s) na Mwenyezi Mungu na kisha onesha jinsi alivyoishinda.

12. Eleza sababu sita zilizosababisha kuporomoka Dola ya Kiislamu aliyoianzisha Mtume (s.a.w).

Scanned by CamScanner